JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 02 - 2020/2021**

**DHIDI YA**

## CARRY MASTORY MEDIA T/A CARRY MASTORY

**SHAURI NA. 02 - 2020/2021**

# UAMUZI

## UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MTANDAONI), 2018

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa maudhui mtandaoni kwa **Carry Mastory**, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mitandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yo yote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mtandaoni au Sheria nyingine.

1.3 Katika tarehe na vipindi tofauti, **Carry Mastory** kupitia Chaneli yake ya YouTube, inatuhumiwa kuchapisha maudhui yenye lugha isiyo na staha na kuhamasisha ufanyaji wa ngono kinyume na maumbile. Pia walichapisha Maudhui yasiyokuwa na mizania ya habari.

1.4 Tarehe 16 Juni, 2020, **Carry Mastory** inatuhumiwa kuwa ilichapisha/iliweka mtandaoni kupitia Chaneli yake ya YouTube maudhui yenye kichwa cha habari **Mambo ya Buza kwa Mpalange/ Vibamia/Wanaume wa Kinondoni/ Kila Mwanamke ana Wanaume wa**

**3/Kiba/ Harmonize,** bila ya kuzingatia Sheria, Kanuni, na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

1.5 Katika picha jongefu hiyo iliyochapishwa tarehe 16 Juni, 2020, mtangazaji wa **Carry Mastory** alikuwa akimhoji mtu aliyejitambulisha kwa jina la **Mr. Misifa** ambapo katika mahojiano hayo, mhojiwa alikuwa akitamka na kushabikia maneno *Buza kwa Mpalange* na kutoa tafsiri yake kwa lugha ya mtaani kwamba ni kufanya mapenzi kinyume na maumbile, jambo ambalo ni kinyume na Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari nchini.

1.6 Katika mahojiano hayo, mtangazaji wa **Carry Mastory** na **Mr. Misifa** waliongea yafuatayo:

***Mr. Misifa:*** *Ukiwa unaenda Buza kwa Mpalange ni mwisho kwa hiyo anamaanisha kwa Mpalange ni nyuma ya Buza, kwamba nyuma ya Buza ni kutamu nadhani wewe mwenyewe hilo neno ukilitafsiri vizuri ushaelewa. Mwanamke ana pande mbili ana mbele na nyuma.*

**Nick Tozi:** *Hivi nikuulize kwanza unajua maana ya kwa Mpalange ni nini? Au kwa Mpalange ni wapi utapata kuyajua.*

**Nick Tozi:** *tukiachana na vichekesho ambavyo umekuwa ukipost lakini vile vile unapostigi kwichkwich zile huwa unafikiriaga nini mzee?*

***Mr. Misifa:*** *Kwichkwich mara nyingi huwa napenda kuwaelimisha wadada, unajua wadada wamekuwa tu wanatoa comments wanaume hawawezi hawawezi lakini je wewe unaweza ndani yake? Unamlaumu mwanaume hakufikishi wewe unamfikisha? Una uhakika gani kama mwanaume amefika kileleni? Wewe unalalamika hufiki je uanaume ungeuvaa wewe ungemfikisha? Umeona kwa hiyo mara nyingi natoa tu elimu hata kwa wanaume natoa pia elimu kwa wanaume wenzangu huwa natoa vitu wanaume mjifunze hapa mtagiane kwa hiyo tunatagiana vile vile.*

**Mr. Misifa:** *Mpalange ni nyuma ya Buza, kwamba nyuma ya Buza ni kutamu nadhani wewe mwenyewe hilo neno ukilitafsiri vizuri utaelewa.*
*Mwanamke ana pande mbili ana nyuma na mbele akikwambia nyuma ni kutamu unakuwa tayari ushapata picha.*

**Nick Toz:** *kwa hiyo kwa Mpalange ni huko...*

**Mr. Misifa:** *Kwa Mpalange ni nyuma ya mwanamke, yaani kwa Mpalange ni nyuma, mwisho au nyuma sijui unanielewa vizuri? Kama ni mwisho au nyuma kwa hiyo akiongea mwanamke kama Jikeshupa kwamba kwa Mpalange ni kutamu tukimchukua Jikeshupa mtu kamweka hapa mbele tukamwangalia wapi ni mbele na wapi ni nyuma utajua nazungumzia sehemu gani.*

1.7 Pia, tarehe 27 Juni, 2020, kupitia Chaneli yao ya YouTube, **Carry Mastory** wanatuhumiwa kuwa walichapisha maudhui ya mkutano wa msanii **Godfrey Tumaini,** maarufu kama **Dudubaya** na Waandishi wa Habari. Katika mkutano huo, **Dudubaya** alitoa kashfa na shutuma dhidi ya Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) na uongozi wake kuwa wanakwamisha sanaa nchini na kushikilia rufaa yake ili aendelee kufungiwa mpaka kampeni zipite. Maudhui hayo yaliyoegemea upande mmoja na yaliyojaa shutuma, kashfa na chuki yalichapishwa bila

kuzingatia Weledi. Maudhui hayo hayakufuata Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari nchini.

1.8 Katika mkutano huo na Waandishi wa Habari, **Dudubaya** aliongea maneno yafuatayo:

***"So kinachofanyika kwanini BASATA ile rufaa yangu kwa Waziri Mwakyembe hata juzi nimeona Juliana Shonza kaongea kwamba Dudubaya hajaja kwangu hajaja kwa Waziri yaani ile rufaa yangu kwa sababu wakati inapokelewa na Wizara ni Baraza la Sanaa ndio inapelekwa wameishikilia palepale,..so kinachoendelea ni kwamba wanifungie mpaka mwakani mpaka kampeni zipite sijui umenielewa hapo...mnanielewa walimwengu?...kwa hiyo hii kampeni Baraza la Sanaa tunaposhindana ni kwamba wanatumika na hawa majizi kwenye Sanaa na hasa hasa kuna watu pale BASATA watatu kama wanne,watano wanatumika kwenye huu mchezo mchafu kwa kukwamisha Sanaa kitu kinachofanya mpaka wasanii kina Lady Jaydee kina Vanessa kina nani..."***

1.9 Vile vile, tarehe 14 Julai, 2020, **Carry Mastory** kupitia Chaneli yao ya **YouTube** waliendelea kurusha na kuchapisha maudhui yaliyojaa shutuma, chuki na kashfa dhidi ya Baraza la Sanaa la Tanzania (BASATA) na Uongozi wake bila kuzingatia mizania kwa kutowapa nafasi watuhumiwa kutolea ufafanuzi tuhuma hizo.

1.10 Katika mahojiano hayo, mwanamuziki **Dudubaya** alitamka maneno yafuatayo:

***"Pale BASATA pale kuna watu kama wawili hivi wana vichwa kama matikiti. Haiwezekani taifa eti mtu anatapeliwa mbele ya Naibu Waziri halafu huyo huyo kiongozi wa BASATA anamsainisha mkataba analiambia lile eti lile jizi analiambia hivi eti nakulipa hela yako ole wako uongee na Waandishi wa habari kwenye taifa huru kuna uhuru gani huyo Meshack huyo mtoto Madam Ritha kamsainisha mkataba mbele ya huyu huyu Mwingereza huyu unamwambia eti mtoto asihojiwe ni siri analipwaje? Ni udikteta gani huu. Baraza la Sanaa kuna watu wengi sana pale lakini kuna innocent people wako pale lakini huyu Mwingereza huyu ndo maana narudia eti kuna siku ananiambia hivi msafishe huyu mama nilimwambia wewe ni mburura ndo maana kichwa kama tikiti huwezi ukanituma nimsafishe mtu mwizi huwezi. Na ndio maana nilishawahi kukaa na watu nikawaambia hii Sanaa inakoelekea watu watakuja kupigana tanchi nafikiri tanchi mnaelewa maana yake..."***

1.11 Aidha tarehe 09 Julai, 2020, **Carry Mastory** walichapisha katika Chaneli yao ya YouTube, mahojiano na mtu aliyejitambulisha kama **Bi. Zai**. Katika mahojiano hayo, mtangazaji wa **Carry Mastory** alimruhusu **Bi. Zai** kutamka maneno yasiyo na staha kinyume na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

1.12 Katika mahojiano hayo **Bi. Zai** alitamka maneno yafuatayo:

***Mtangazaji:*** *Nitajie sifa mbili za Mmakonde kwanza.*

***Mhojiwa:*** *Mmmmmh...ufundi kitandani. Ahhh mmmh na mtafutaji hakuna Mmakonde mvivu mvivu.*

***Mtangazaji:*** *Asa wamakonde mafundi kitandani mbona shemeji yetu kakubwaga.*

***Mhojiwa:*** *Sijawahi kuachwa nikikuchoka natoka mwenyewe tuu.*

***Mtangazaji:*** *Bwana Stan alikimbia Bwana Stan Bakora bwana akakimbia huna lolote kitandani.*

***Mhojiwa:*** *Sijawahi kuwa na mahusiano na Stan Bakora ni mshikaji wangu sana sijawahi kuwa na mahusiano nae.*

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kitendo cha kuchapisha na kutangaza maudhui yasiyo na staha na yanayoshabikia ufanyaji wa ngono kinyume na maumbile, yenye shutuma, matusi na kashfa na yasiyozingatia mizania ya habari, **Carry Mastory** inatuhumiwa kukiuka Kanuni Na. 5 (1) (a), (b), 7(1) (a) (b), 12 (b) (c) na (k) (i) (ii) (iii) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018. Kanuni tajwa zinasomeka kama ifuatavyo:

*5-(1) For the purpose of these Regulations, an online content provider shall have the obligations to-*
- *(a) ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law;*
- *(b) take into account trends and cultural sensitivities of the general public.*

*7-(1) A licencee of online radio and television intended for broadcasting over the public internet with the objective of informing, entertaining and educating the public shall adhere to the following conditions:*
- *(a) content streamed to abide to regulations governing the broadcasting services;*
- *(b) adhere to journalism ethics and professionalism.*

*12.-Online content services provider shall not publish-*
- *(b) obscene content*
- *(c) hate speech*
- *(k) content that uses bad language including-*
  - *(i) the use of disparaging or abusive words which is calculated to offend an individual or a group of persons;*
  - *(ii) crude references words, in any language commonly used in the United Republic, which are considered obscene or profane including crude references to sexual intercourse and sexual organs;*
  - *(iii) hate speech.*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI

Tarehe 27 Julai, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Carry Mastory,** wito wa kuwasilisha utetezi wao wa maandishi pamoja na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui kujieleza dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

Tarehe 03 Agosti, 2020, Uongozi wa **Carry Mastory** uliwasilisha utetezi wa maandishi uliosainiwa na **Catherine Ngowo**, Mkurugenzi wa **Carry Mastory.** Pia, tarehe 05 Agosti, 2020, Uongozi huo ukiwakilishwa na **Catherine Ngowo**, Mkurugenzi wa **Carry Mastory**, pamoja na **Gervas Andrew**, Meneja wa Uendeshaji wa Kituo ulifika mbele ya Kamati kutoa utetezi.

## 4.0 KUSOMEWA SHTAKA, KUANGALIA NA KUSIKILIZA MAUDHUI YA CARRY MASTORY

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **Carry Mastory** shitaka lao. Pia, Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Carry Mastory** waliangalia na kusikiliza maudhui yaliyochapishwa na kutangazwa na **Carry Mastory** katika tarehe tajwa hapo juu na kisha kuualika Uongozi huo kujitetea ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni au la.

## 5.0 UTETEZI WA CARRY MASTORY

Katika maelezo yao ya maandishi**, Carry Mastory** wamekiri mashtaka yao yote, wameomba radhi na kuahidi kutorudia kosa. Wamesema kuwa kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili na kwa kutambua wajibu walionao kwa jamii, Taifa na tasnia ya habari, wamefanya maboresho na kuchukua hatua za kiutendaji ili kuhakikisha hawakiuki tena Sheria na Kanuni.

Waliendelea kusema kuwa wameyafuta maudhui yaliyokiuka Kanuni katika Chaneli yao kabla ya kupokea barua ya wito wa Kamati. Pia wamepanga kushirikiana na wadau wa masuala ya Sheria ili kutoa mafunzo ya Sheria kuhusu Maudhui Mtandaoni kwa watangazaji na wafanyakazi wao kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Agosti ili kuwajengea watendaji wao uelewa katika Kanuni za Utangazaji. Vile vile, wamesema kuwa wameboresha utaratibu wa kuhakiki maudhui kabla ya kuyachapisha au kuyatengeneza. Hatua hii imeenda sambamba na uimarishaji wa udthibiti wa maudhui kabla ya kurushwa hewani. Walimalizia kwa kuiomba Kamati iwasamehe na iendelee kuwalea.

5.1 Katika utetezi wao wa mdomo walisema kuwa Kituo chao ni kichanga na kwamba wanapitia changamoto nyingi na kubwa na hivyo wataajiri mtu wa kuyasimamia vizuri maudhui kabla ya kuchapishwa. Walidai kuwa msanii **Dudubaya** amekuwa akiwalazimisha kuchapisha maudhui yake na wasipofanya hivyo, huwa anawachafua mitandaoni.

5.2 Walisisitiza kuwa Vituo vya Maudhui Mtandaoni vinapitia changamoto za vitisho na kashfa kutoka wasanii kama **Dudubaya.** Walipoulizwa na Kamati, kama walitoa tarifa Polisi kuhusu kutishiwa na wasanii kwa vile ni kosa la jinai walijibu kuwa hawajafanya hivyo. Pia, walidai kuwa wao

kama vijana wanapitia changamoto za kuwepo kwa misemo mbali mbali mitaani, ambapo kwa kukosa kwao uelewa wanaona ni maneno ya kawaida. Kuhusu kosa la kutozingatia mizania ya habari, walidai kuwa siku kadhaa baada ya kuchapisha maudhui yale, waliamua kufanya mahojiano na BASATA ambao walilitolea ufafanuzi suala lile.

Wlihitimisha utetezi wao kwa kusema kuwa tayari wameshakaa na wafanyakazi wao ili kuwaonya na kuwaelimisha kuhusu Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

Katika tathmini yake Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Carry Mastory** imetenda makosa ya kuchapisha na kutangaza maudhui yasiyo na staha na yanayoshabikia ufanyaji wa ngono na mapenzi ya kinyume na maumbile kwa makusudi kama walivyokiri wenyewe;

6.2 Kulikuwa na ukiukaji mkubwa wa Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari katika uwasilishwaji wa Maudhui yao pamoja na maneno yaliyotumika. Maudhui yao pia yalilenga kuhamasisha ufanyaji wa vitendo ambavyo havikubaliki kwa mujibu wa Maadili na Utamaduni wa Kitanzania;

6.3 Kuwa hoja ya uchanga wa Kituo chao iliyotolewa na **Carry Mastory** haina mashiko kwa sababu wao kama chombo cha habari wana wajibu wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari;

6.4 Kamati ya Maudhui imejiridhisha kuwa **Carry Mastory** wana udhaifu mkubwa katika maandalizi/utayarishaji, usimamizi na uhariri/uhakiki wa maudhui yao. Vile vile, wafanyakazi wake wanauelewa mdogo wa Sheria na Kanuni zinazosimamia chombo chao;

6.5 Kamati ya Maudhui imeona hoja ya **Carry Mastory** kuwa vyombo vya habari vina changamoto ya misemo/maneno mbali mbali yanayoibuka mitaani haina mashiko kwa sababu wana wajibu wa kufanya uchaguzi sahihi wa maneno yanayozingatia Sheria na Kanuni kabla ya kuyatumia kwenye maudhui yao. Sio kila misemo/maneno ya mitaani yanafaa kutumika kwenye chombo cha habari;

6.6 **Carry Mastory** imetenda kosa la kutangaza maudhui yenye shutuma, matusi na kashfa na yasiyozingatia mizania ya habari dhidi ya BASATA kwa makusudi kwani Sheria, Kanuni na madili ya fani zinawataka kutoa fursa kwa BASATA kutolea ufafanuzi tuhuma dhidi yao walizozitangaza dhidi yao;

6.7 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa **Carry Mastory** kuwa siku kadhaa baada ya kutangaza maudhui yenye shutuma dhidi ya BASATA,

waliwapa BASATA nafasi kutolea ufafanuzi shutuma zile, hauna mashiko kwa sababu Sheria na Kanuni zinawataka wangewapa BASATA nafasi katika kipindi kile kile walichotumia kutangaza shutuma dhidi yao. Utangazaji wa maudhui bila ya kuzingatia mizania ya habari ni kosa kubwa la kiweledi na kimaadili katika Uandishi na Utangazaji wa Habari;

6.8 Kamati imeona kuwa utetezi wa **Carry Mastory** kuwa huwa wanapata vitisho na kashfa kutoka kwa wasanii kama **Dudubaya** wasipotangaza maudhui yao hauna mashiko kwa sababu wao kama chombo cha habari, chenye dhamana ya kuistawisha jamii, wanapaswa kuchagua kuzingatia Sheria na Kanuni zaidi kuliko kuogopa vitisho/kashfa ili kuepuka kutangaza maudhui yanayomomonyoa madili ya jamii kwa kisingizio cha vitisho/kashfa. **Carry Mastory** pia wameshindwa kuthibitisha kama wameshawahi kuripoti vitisho na kashfa hizo wanazodai katika vyombo vya ulinzi na usalama;

6.9 Hivyo, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Carry Mastory** imetenda makosa ya kutangaza maudhui yasiyo na staha na yanayoshabikia ufanyaji wa ngono na mapenzi ya kinyume na maumbile, yenye shutuma, matusi na kashfa na yasiyozingatia mizania ya habari kinyume na Kanuni Na. 5 (1) (a), (b), 7(1) (a) (b), 12 (b) (c) na (k) (i) (ii) (iii) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018.

## 7.0 USHAURI WA KAMATI KWA CARRY MASTORY

Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Carry Mastory** kuimarisha utayarishaji, usimamizi na uhariri wa maudhui yao ili kuepuka utangazaji wa maudhui yanayovunja Sheria, Kanuni, Weledi na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari;

Pia, **Carry Mastory** wanashauriwa kuhakikisha wanawapatia watangazaji wao mafunzo ya mara kwa mara kuhusu Sheria, Kanuni na madili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari kuepuka makosa.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kuutafakari kwa kina utetezi uliotolewa na Uongozi wa **Carry Mastory**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **Carry Mastory** kupitia Chaneli yake ya YouTube wamekiuka Kanuni tajwa za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018.

Hivyo basi, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **Carry Mastory:**

1. Wanapewa Onyo Kali;

2. Wanawekwa chini ya uangalizi kwa muda wa miezi sita (6) pamoja na kutahadharishwa kuwa hatua kali zaidi za kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi yao iwapo hawatajirekebisha ndani ya muda tajwa;

3. Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00)** tu, itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam, leo tarehe **14 Agosti, 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Joseph Method Mapunda**

............................................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S.L.P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Abdul Ramadhani Ngarawa**..................................

2. **Derek Kaitira Murusuri**....................................

3. **Jacob Gregory Tesha**.........................................